حرمين

رئاسة الشؤون الدينية
بالمسجد الحرام والمسجد النبوي

# SIFA YA 'UMRA

## Pamoja na Dua Zilizochaguliwa

Machapisho ya Qaasid
Al-Haramayn Ash-Sharifayn

مطبوعات قاصد الحرمين الشريفين

برنامج قاصد الحرمين

# SIFA YA ‘UMRA

## Pamoja na Dua Zilizochaguliwa

Machapisho ya Qaasid Al-Haramayn
Ash-Sharifayn

مطبوعات قاصد الحرمين الشريفين

ⓗ رئاسة الشؤون الدينية بالمسجد الحرام والمسجد النبوي، ١٤٤٦هـ

رئاسة الشؤون الدينية بالمسجد الحرام والمسجد النبوي
صفة العمرة باللغة السواحلية./رئاسة الشؤون الدينية بالمسجد الحرام والمسجد النبوي - ط١. .- مكة المكرمة، ١٤٤٦هـ
٣١ص، ١٤×٢١سم
رقم الإيداع: ١٤٤٦/١٤١٦٤
ردمك: ٩٧٨-٦٠٣-٨٥٠٦-٦٠-٨

**Machapisho ya Qasid Al-Haramayn Ash-Sharifayn**

**Toleo la Kwanza**
١٤٤٦هـ/٢٠٢٥م

بسم الله الرحمن الرحيم

# Utangulizi mku

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu, rehema na amani ziwe juu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, na kwa ahli zake, masahaba wake, na wale waliomfuata. Ama baad:

Kwa kuwa Allah Ta'ala amefanya Al-Bayt Al-Haram kuwa Qibla inalokusanya nyoyo na miili ya Waislamu, na kuwa mwongozo kwa walimwengu, na hifadhi yenye amani inayothibitisha ufanisi wa watu katika maisha yao na marejeo yao.

Na katika kila mwaka mamilioni ya Waislamu huwasili katika mji mtukufu wa Makkah wakibeba matumaini yao, hisia zao, na dua zao. Pia huja na maswali kuhusu wajibu wao katika dini yao na ibada zao.

Kwa muktadha huu, kuitukuza Al-Masjid Al-Haram, kuwaheshimu watu wake na wageni wake ni wajibu na jukumu kubwa. Uongozi wa Masuala ya Kidini ya Msikiti Mtakatifu na Msikiti wa Mtume umepewa heshima ya kubeba jukumu hili na kulitekeleza kwa ukamilifu wake.

Machapisho haya ya "Qaasid Al-Haramayn Ash-Sharifayn" ni uthibitisho wa dhati wa hisia za watu wa ardhi hii tukufu na wale wanaohudumu katika Msikiti Mtakatifu kwa wageni wa Mwenyezi Mungu. Ni zawadi yenye thamani kwa wageni wa

Nyumba ya Allah, ambayo wataibeba wakiwa na fahari wanaporudi makwao.

Kwa hivyo, “Uongozi wa Masuala ya Kidini wa Msikiti Mtakatifu na Msikiti wa Mtume” unawasilisha kijitabu hiki cha mwongozo kwa ndugu zetu wageni. Kinaelezea sifa ya ‘Umra kwa nguzo zake, wajibu wake, suna zake, na mambo yaliyokatazwa katika Ihram, pamoja na dua zilizochaguliwa kwa ajili ya Waislamu kuzitumia wakati wa ‘Umra yao. Inatarajiwa kutoka kwa ndugu zetu Waislamu wajifunze kwa kina dini yao, na wamshukuru Mola wao Mtukufu aliyewarahisishia kutembelea Nyumba Yake Tukufu na kutekeleza ibada zao kwa utulivu na wepesi.

Mwenyezi Mungu atukubalie sisi na nyinyi matendo mema. Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu, na rehema na amani ziwe juu ya Mtume wetu Muhammad, familia yake, na maswahaba wake wote.

**Uongozi wa Masuala ya Kidini wa Msikiti Mtakatifu na Msikiti wa Mtume**

# Utangulizi

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu, tunamhimidi, tunamtaka msaada, tunamwomba msamaha, na tunajilinda kwa Mwenyezi Mungu dhidi ya shari za nafsi zetu na maovu ya matendo yetu. Mwenyezi Mungu akimwongoza mtu, hakuna wa kumpoteza, na akimpoteza mtu, hakuna wa kumwongoza. Ninamshuhudia kuwa hakuna Mungu mwingine anayestahili kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake, hana mshirika, na ninashuhudia kuwa Muhammad (SAW) ni mja na Mtume wake. Ama baad:

kijitabu hiki kimetolewa ili kiwe msaada kwa wageni na na waumini wanaotekeleza ibada yao ya Umrah kwa mujibu wa dalili za Qur'an na Sunnah, pamoja na maneno ya wanazuoni wa Kiisilamu. Kimetolewa ili kuboresha uzoefu wa wageni kwa msingi wa kushirirkiana katika wema na ucha Mungu panoja na kusambaza elimu. kwa mujibu wa dalili ya Qur'an na Sunnah, pamoja na maneno ya wanazuoni wa Kiisilamu. Hiki ni kijitabu kidogo lakini chenye manufaa makubwa katika kueleza sifa na hukumu za Umrah. Kwa kuwa Umrah inaruhusiwa wakati wote wa mwaka, unahitaji kujua hukumu zake na taratibu zake ni endelevu na ni wa mara kwa mara, tofauti na Hajj ambayo ina muda maalum. Tumekitoa kwa kueleza sifa za Umrah, kisha tukafuatisha na maombi

(dua) kutoka katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunnah sahihi.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu abariki kazi hii na aifanye kwa ajili ya kutaka radhi zake, yenye manufaa kwa waja wake wa Kiisilamu. Na rehma na amani zimfikie Mtume wetu Muhammad.

# Miakaati na Ihramu

Miakaati ni maeneo ambayo mtu anapaswa kuingia katika hali ya Ihramu endapo ananuia kufanya Umrah.

Sunnah imebainisha maeneo maalum ambapo hairuhusiwi kwa yeyote anayepitia hapo akiwa na nia ya Umrah kuvuka isipokuwa akiwa katika hali ya Ihramu. Maeneo hayo ni matano:

**Dhul-Hulaifah:** Sasa inajulikana kama Abar Ali. Ni Mpaka wa watu wa Madinah na yeyote anayepita hapo. Iko umbali wa takribani 420 km kutoka Makkah.

**Al-Juhfah:** Ni kijiji karibu na Rabigh, na ni Mpaka wa watu wa Sham, Misri, Magharibi ya Afrika, na yeyote anayepita hapo. Iko umbali wa takribani 186 km kutoka Makkah. Watu wengi huweka Ihramu Rabigh.

**Qarn al-Manazil:** Inajulikana pia kama As-Sail al-Kabir. Ni Mpaka wa watu wa Najd, Taif na yeyote anayepita hapo. Iko umbali wa takribani 78 km kutoka Makkah. Wadi Muharram, ulio upande wa juu wa Qarn al-Manazil kutoka barabara ya Hada, ni Miakaati mbadala na iko umbali wa 75 km kutoka Makkah.

**Yalamlam:** Ni Mpaka wa watu wa Yemen na yeyote anayepita hapo. Iko umbali wa takribani 120 km kutoka Makkah.

**Dhat Irq:** Inajulikana pia kama Adh-Dharibah. Ni Mpaka wa watu wa Iraq na yeyote anayepita hapo. Iko umbali wa takribani 100 km kutoka Makkah.

Mtu ambaye anakaa ndani ya mipaka ya Miakaati hiyo anaweza kuingia katika Ihramu kutoka nyumbani kwake. Watu wa Makkah wana Ihramu kutoka nje ya mipaka ya Haram kwa Umrah, lakini kwa Hajj wanaweza kuingia Ihramu kutoka makazi yao.

# Tanbihi (Uzinduzi)

Anayefika kwa ndege kwa nia ya Hajj au Umrah anatakiwa kuingia katika Ihramu anapokaribia mmojawapo wa mipaka Mipaka. Haifai kuchelewesha Ihramu hadi afike Uwanja wa Ndege wa Jeddah kwa sababu Jeddah si Miakaati isipokuwa kwa wakazi wake.

Ikiwa hana mavazi ya Ihramu, anapaswa kuacha suruali, avue shati lake na kulivaa mabegani mwake, kisha aweke nia ya Ihramu. Baada ya kutua, anavaa mavazi ya Ihramu mara tu anapoyapata na kuondoa suruali yake.

Kwa wanawake, hakuna vazi maalum la Ihramu. Wanavaa mavazi yao ya kawaida lakini kama wanavaa burqa au niqab, wanapaswa kuvua na kufunika nyuso zao kwa ushungi mbele ya wanaume wasio maharimu.

# Nguzo, Wajibu na Sunnah za Umrah

**Nguzo za Umrah:**

1. Nia ya kuingia katika ibada (Ihramu).
2. Kutufu Al-Kaaba.
3. Kusai kati ya Safa na Marwa.

- Mtu akiacha nguzo yoyote, Umrah yake haitokubaliwa mpaka aitimize kwa mujibu wa sharia.

**Wajibu wa Umrah:**

- Ihramu inatakiwa kufanywa kutoka kwenye miqat kwa yule anayepita hapo. Kwa yule ambaye makazi yake yako ndani ya mipaka ya miqat, ihramu yake itakuwa pale anapoianza. Ama kwa Mkaaji wa Makkah, inampasa kutoka hadi sehemu ya Hilli kwa ajili ya umra.
- Kunyoa au kupunguza nywele.
- Mtu akiacha wajibu wa Umrah kwa makusudi, atapata dhambi na anapaswa kutoa fidia. Ikiwa ameacha bila kukusudia, basi anatakiwa kutoa fidia pekee.

**Sunnah za Umrah:**

- Kila kilicho nje ya nguzo na wajibu ni Sunnah, kama vile kufunua bega la kulia wakati wa Tawaf (Idtiba) na kutembea kwa haraka (Ramal) katika mizunguko mitatu ya kwanza ya Tawaf.
- Mtu akiacha Sunnah, hana dhambi, lakini hupoteza fadhila zake.

# Mambo Yanayoharamishwa Wakati wa Ihramu

**Yamegawanyika katika sehemu tatu:**

**Moja:** Mambo yalioharamishwa kwa wanaume na wanawake:

1. Kunyoa nywele au kukata kucha.
2. Kutumia manukato.
3. Kuvaa glovu.
4. Kufanya posa, kwa binafsi yake au kwa mtu mwingine.
5. Kufanya tendo la ndoa.
6. Kuwinda wanyama wa porini au kusaidia kuwinda akiwa anahirimia.

**Pili:** Mambo yalioharamishwa kwa wanaume pekee:

1. Kuvaa nguo zilizoshonwa.
2. Kufunika kichwa kwa kitu kinachogusa ngozi.

**Tatu:** Mambo yalioharamishwa kwa wanawake pekee:

1. Kufunika uso kwa burqa au niqab, lakini wanapaswa kujifunika kwa ushungi mbele ya wanaume wasio maharimu.

Hukumu ya Anayevunja Sheria za Ihramu:

- Akiwa hajui, amesahau au amelazimishwa, hana dhambi wala fidia.

- Akitenda kwa dharura, anaruhusiwa lakini anatakiwa kutoa fidia.
- Akitenda bila udhuru, anapata dhambi na anatakiwa kutoa fidia.

Sehemu za Makatazo ya Ihramu kwa Mujibu wa Fidya:

**Kwanza:** Katika kuondoa nywele na kucha, kutumia manukato, kuvaa glovu, kuvaa nguo zilizoshonwa kwa wanaume, kufunika kichwa kwa wanaume, mwanamke kuvaa nikabu, na kushikana kimapenzi kwa shahawa, kwa kila moja kati ya makatazo haya, mtu ana hiari kati ya mambo matatu:

A. Kufunga siku tatu mfululizo au bila mfululizo.

B. Kuwalisha masikini sita, kila mmoja nusu saa' ya chakula kama tende, mchele au kinginecho.

C. Kuchinja mbuzi na kugawa kwa masikini wa Haram.

**Pili:** Anayeacha mojawapo ya wajibu wa Umra, kama kuhirimia kutoka miqat, basi lazima achinje fidya inayokubalika kwa dhabihu, iwe dume au jike kutoka kwa kondoo au mbuzi, kisha agawe nyama yote kwa masikini wa Haram na asile chochote.

**Tatu:** Fidya ya kujamiana (tendo la ndoa): Anayeingiliana kabla ya sa'yi, Umra yake huharibika, na analazimika kuimaliza kisha kuilipa, na pia kuchinja (fidya). Ikiwa hawezi, atafunga siku kumi.

Anayeingiliana baada ya sa'yi lakini kabla ya kunyoa au kukata nywele, Umra yake haiharibiki, lakini lazima achinje (fidya). Ikiwa hawezi, atafunga siku kumi.

**Nne:** Adhabu ya kuwinda, nayo ina hali mbili:

- Ikiwa windo lina mfano kutoka mnyama wa mifugo, basi ana hiari kati ya mambo matatu:
  - A. Kuchinja mnyama anayefanana na windo na kugawa kwa masikini wa Haram.
  - B. Kuangalia thamani ya windo hilo, kisha anunue chakula kwa thamani hiyo na agawe kwa masikini, kila mmoja nusu saa' ya chakula.
  - C. Kufunga kwa kila masikini siku moja.
- Kiwa windo halina mfano wa wanyama, kama nzige, basi ana hiari kati ya mambo mawili:
  - A. Kuangalia thamani ya windo na kutoa chakula kwa thamani hiyo kwa masikini, kila mmoja nusu saa'.
  - B. Ima afunge kwa kila masikini siku moja.

## Sifa ya Umra

- Wakati wa kufika kwa anayetaka kufanya Umra akiwa kwenye miqat:

Inapendekezwa kuoga na kutumia manukato kabla ya ihramu.

Mwanaume avae izari na ridai, inapendekezwa ziwe nyeupe na safi.

Mwanamke avae mavazi ya heshima anavyotaka, lakini asivae nikabu wala glovu.

Atie nia moyoni kuingia katika ibada, na ni sunna kusema: "*Labbayka 'Umrah*" au "*Allahumma Labbayka 'Umrah*".

Ikiwa ana hofu ya kushindwa kutimiza ibada ya Umra kutokana na ugonjwa au hofu ya adui, inapendekezwa kusema: "*Fa-in habasani haabis famahilli haythu habastani*" ili aweze kutoka kwenye ihramu bila malipo ikiwa atazuiliwa.

Ni sunna kuongeza talbiya na kuitamka kwa sauti wakati wa safari kuelekea Makka.

- Mambo anayofanya mwenye kutaka kufanya Umra anapoingia Msikiti Mtakatifu:

Anapoingia, ni sunna kuweka mguu wa kulia mbele na kusema:

"*Bismillah, wa-salatu wa-salamu 'ala Rasulillah*"

(Imepokewa na Ibn Majah). "*A'udhu billahil-'azhim wa biwajhihil-karim wa bi-sultanihil-qadim minash-shaytanir-rajim*" (Imepokewa na Abu Dawud).

"*Allahummaftah li abwaba rahmatik*" (Imepokewa na Muslim).

Atakaribia Hajar Aswad ili kuanza tawafu, akiweza, aiguse kwa mkono wa kulia na kuibusu. Ikiwa hawezi, basi aibusu mkono wake ikiwa ameigusa kwa mkono wake. Ikiwa hawezi kugusa, basi aikabili na kuashiria kwa mkono bila kuibusu. Ni bora asisukume watu.

Atasema "*Bismillah, Allahu Akbar*" wakati wa kugusa Hajar Aswad.

Atazunguka Kaaba kwa kuanzia upande wa kulia, akiiweka upande wake wa kushoto. Atakapofika Rukn Yamani, ataugusa bila kuubusu wala kuinua mkono, na atasema kati ya Rukn Yamani na Hajar Aswad: Na katika wao wapo wanaosema: "Mola wetu Mlezi, tupe duniani mema, na Akhera mema, na utulinde na adhabu ya Moto!" [Al-Baqarah: 201].

Atafanya idtiba' (kuweka bega la kulia wazi) katika tawafu yote. Akimaliza Tawafu atafinika bega lake.

Atakwenda haraka katika mizunguko mitatu ya kwanza (ramal).

Baada ya tawafu saba, ataswali rakaa mbili nyuma ya Maqam Ibrahim, akisoma Suratul-Kafirun kwenye rakaa ya kwanza na Suratul-Ikhlas kwenye rakaa ya pili.

Baada ya swala, ni sunna kunywa maji ya Zamzam na kugusa Hajar Aswad tena ikiwa ataweza.

Kuelekea Safa na Marwa: Atakapokaribia Safa atasoma: Hakika vilima vya Safaa na Marwa ni katika alama za Mwenyezi Mungu. Basi anayehiji kwenye Nyumba hiyo au akafanya Umra, si kosa kwake kuizunguka. Na anayejitendea mwenyewe kheri basi bila ya shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye shukrani na Mjuzi. [Al-Baqarah: 158] Huisoma aya hii anapokaribia Safa kabla ya kupanda mlima, wala haisomi isipokuwa katika sehemu hii tu, na mwanzoni mwa duru ya kwanza pekee, wala hairudii katika kila duru.

Atapanda Safa na kuelekea Qibla, akisema "*Allahu Akbar*", akiinua mikono, kisha atasema: "*La ilaha illa Allah wahdahu la sharika lahu, lahul-mulku walahul-hamdu, wa huwa 'ala kulli shay'in qadir, la ilaha illa Allah wahdahu, anjaza wa'dahu, wa nasara 'abdahu, wa hazama al-ahzaba wahdahu*" (Maratatu tatu). Kisha aombe anachotaka.

Kisha anashuka kutoka Safa akielekea Marwa, akitembea kwa kawaida huku akimtaja Mwenyezi Mungu na kuomba dua kwa yale yanayomjia kwa wepesi—kwa ajili yake, familia yake, na wale anaowapenda—mpaka anapofika kwenye alama ya kijani, ndipo anakimbia kwa kasi kadri awezavyo hadi kufikia alama nyingine ya kijani. Baada ya hapo, anaendelea kutembea kwa kawaida hadi anapopanda

Marwa. Akifika Marwa na kupanda, anakabiliana na Qibla na kusema kile alichosema akiwa Safa.

Hufanya sa'ii mara saba; kutoka Safa hadi Marwa ni mzunguko mmoja, na kutoka Marwa hadi Safa ni mzunguko wa pili. Anapofika kati ya alama mbili za kijani, anakimbia, bila kudhuru watu waliomzunguka. Anaendelea hivyo hadi akamilishe mizunguko saba.

Baada ya hapo, ananyoa kichwa chake au anakipunguza, na mwanamke hukusanya nywele zake na kukata kiasi cha ncha ya kidole.

Kwa hayo, Umra inakuwa imekamilika, na mtu anarudi katika hali ya kawaida, akiruhusiwa kufanya yale yote yaliyozuiliwa wakati wa ihramu.

Mwenyezi Mungu amfikishie rehma na amani Mtume wetu Muhammad, pamoja na ahli zake na maswahaba wake wote kwa jumla.

## Dua zilizochaguliwa

**Ee Mwenyezi Mungu,** sifa njema zote ni zako, sifa nyingi, njema, na zenye baraka, kama unavyopenda na kuridhia. Sifa ambazo haziishi wala zisizo na kikomo, kiasi cha mbingu zako, ardhi zako, na vyote unavyotaka baada ya hayo. Kiasi cha wale wanaokusifu na idadi ya wale waliosahau kukutaja. Na rehma na amani ziwe juu ya mja wako na Mtume wako Muhammad, mtume wa mwisho, mteule wako kati ya viumbe vyako, mwaminifu wa wahyi wako, na juu ya ahli zake na maswahaba wake wote.

**Ee Mwenyezi Mungu,** sifa njema zote ni zako, wewe ni Nuru ya mbingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake. Sifa zote ni zako, wewe ndiye Msimamizi wa mbingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake. Sifa zote ni zako, wewe ni haki, ahadi yako ni haki, maneno yako ni haki, kukutana nawe ni haki, Pepo ni haki, Moto ni haki, Saa (ya Kiyama) ni haki, Mitume ni haki, na mtume Muhammad ni haki.

**Ee Mwenyezi Mungu,** nimejisalimisha kwako, nimetegemea kwako, nimekuamini, nimerudi kwako, nimepinga kwa ajili yako, na nimehukumu kwako. Nisamehe dhambi zangu za awali na za baadaye, zile nilizozifanya kwa siri na kwa dhahiri. Wewe ndiye wa kwanza na wa mwisho, hakuna Mungu ila wewe, na hakuna nguvu wala uwezo ila kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

**Ee Mwenyezi Mungu,** nipe nafsi yangu uchaji wake, na itakase, kwani wewe ndiye bora wa kuitakasa, wewe ni mlinzi wake na Mola wake.

**Ee Mwenyezi Mungu,** najikinga kwako na elimu isiyofaa, na moyo usiokuwa na unyenyekevu, na nafsi isiyoridhika, na dua isiyojibiwa.

**Ee Mwenyezi Mungu,** nakuomba kwa sababu sifa njema zote ni zako, hakuna mungu ila wewe, Muumba wa mbingu na ardhi, Mwenye Utukufu na Heshima, Aliye Hai, Aliyesimama kwa uendeshaji wa kila kitu, unisamehe na unirehemu. Na ikiwa umepanga maangamizo kwa watu fulani, nichukue kwako nikiwa sina fitina.

**Mola wetu,** tupe duniani mema, na Akhera mema, na utulinde na adhabu ya Moto.

**Mola wetu,** tumeamini, basi tusamehe na uturehemu, kwani wewe ndiye bora wa kurehemu.

**Mola wetu,** usizipotoshe nyoyo zetu baada ya kutuongoza, na utupe rehema kutoka kwako, hakika wewe ndiye Mwenye kutoa sana.

**Mola wetu,** usituchukulie iwapo tutasahau au tukakosea. Mola wetu, usitubebeshe mzigo kama ule uliowabebesha waliokuwa kabla yetu. Mola wetu, usitubebeshe tusiyoweza kuhimili, tusamehe, utughufirie, na uturehemu. Wewe ndiye Mlinzi wetu, basi tunusuru dhidi ya watu makafiri.

**Mola wangu,** mtekelezaji wa Swala na miongoni mwa kizazi changu, Mola wetu, ukubali dua yangu. Mola

wetu, nisamehe mimi, wazazi wangu, na waumini wote Siku ya Hesabu.

**Mola wetu,** tupe wake na watoto wetu wawe baraka machoni mwetu, na utufanye viongozi wa wacha Mungu.

**Mola wetu,** tupe rehema kutoka kwako na utengeneze mambo yetu kwa uongofu.

**Mola wetu,** tupe yale uliyowaahidi mitume wako, na usituangamize Siku ya Kiyama, hakika wewe huhalifu ahadi.

**Ee Mwenyezi Mungu,** nakuomba uongofu, uchaji Mungu, usafi, na utajiri.

**Ee Mwenyezi Mungu,** nigawie miongoni mwa khofu yako kiasi kitakachonizuia nisikufanyie maasi, na miongoni mwa utiifu wako kinachonifikisha Peponi, na miongoni mwa yakini kinachofanya shida za dunia kuwa nyepesi.

**Ee Mwenyezi Mungu,** nifurahishe kwa kusikia kwangu, kuona kwangu, na nguvu zangu kwa muda wote nitakaoishi, na vifanye viwe urithi wangu. Nisaidie dhidi ya wale wanaonidhulumu na wanaoniadhibu. Usifanye matatizo yangu yawe katika dini yangu. Usifanye dunia iwe lengo langu kuu wala upeo wa elimu yangu. Na usifanye moto uwe sehemu yangu ya mwisho. ifanye pepo iwe ni makazi yangu, wala usinipeane kwa madhambi yangu kwa yule asiyekuogopa wala kunirehemu. Kwa rehema zako, ewe Mwenye rehema kuliko wote.

**Ee Mwenyezi Mungu,** najikinga na Azma yako—hakuna mungu ila wewe—usiwe sababu ya kupotoka kwangu. Wewe ndiwe Aliye Hai, usiyekufa, lakini majini na watu wote watakufa.

**Ee Mwenyezi Mungu,** Muumba wa mbingu na ardhi, Mjuzi wa yaliyofichika na yaliyodhahiri, hakuna Mungu ila wewe, Mola wa kila kitu na Mmiliki wake. Najikinga kwako na shari ya nafsi yangu na shari ya shetani na ushirikina wake, na nisijifanyie madhambi au kumfanyia mwingine.

**Ee Mwenyezi Mungu,** rekebisha dini yangu inayolinda mambo yangu, na rekebisha dunia yangu inayokuwa maisha yangu, na rekebisha Akhera yangu ninayoelekea.

**Ee Mwenyezi Mungu,** nakuomba afya njema duniani na Akhera.

**Ee Mwenyezi Mungu,** nifunike aibu zangu na nipe amani dhidi ya hofu zangu.

**Ee Mwenyezi Mungu,** nihifadhi kutoka mbele yangu, nyuma yangu, kuliani kwangu, kushotoni kwangu, na kutoka juu yangu, na najikinga na adhama yako nisichukuliwe kutoka chini yangu.

**Ee Mwenyezi Mungu,** bora ya mwisho wangu iwe nzuri katika mambo yote, na uniokoe na fedheha ya dunia na adhabu ya Akhera.

**Ee Mwenyezi Mungu,** nisaidie kukutaja, kukushukuru, na kukuabudu kwa njia bora.

**Ee Mwenyezi Mungu,** najikinga kwako na neema yako isiondoke, na badiliko la afya yako, na ghadhabu yako ya ghafla, na adhabu yako.

**Ee Mwenyezi Mungu,** wewe ni mwingi wa kusamehe, unapenda kusamehe, basi nisamehe.

**Ewe Mola,** naomba kwako kheri zote, za sasa na za baadaye, zile ninazozijua na zile nisizozijua. Na najikinga kwako na shari zote, za sasa na za baadaye, zile ninazozijua na zile nisizozijua.

**Ewe Mola,** naomba kwako kheri aliyokuomba mja wako na Mtume wako Muhammad (SAW), na najikinga kwako na shari aliyotaka kujikinga nayo mja wako na Mtume wako Muhammad (SAW).

**Ewe Mola,** naomba kwako Pepo na vitendo vinavyokaribisha kwayo, iwe kwa maneno au kwa vitendo, na najikinga kwako na Moto na vitendo vinavyokaribisha kwayo, iwe kwa maneno au kwa vitendo.

**Ewe Mola,** naomba kwako rehema zako, msamaha wako wa kudumu, faida kutoka kwa kila wema, usalama dhidi ya kila dhambi, ushindi wa Pepo, na uokovu kutoka Motoni.

**Ewe Mola,** nikinge na tabia mbaya, matendo mabaya, tamaa mbaya, na maradhi mabaya.

**Ewe Mola,** nisamehe dhambi zangu zote, na uniongoze kwenye tabia njema, hakuna wa kuongoza kwenye tabia njema ila Wewe, na niepushe na tabia mbaya, hakuna wa kuzuia tabia mbaya ila Wewe.

**Ewe Mola,** naomba kwako uchaji wako wakati wa faragha na hadhara, naomba kwako neno la haki katika hasira na ridhaa, naomba kwako wastani katika umaskini na utajiri, naomba kwako neema isiyoisha, furaha ya moyo isiyo na kikomo, ridhaa baada ya hukumu yako, maisha mazuri baada ya mauti, ladha ya kutazama uso wako mtukufu, na shauku ya kukutana na Wewe, bila madhara wala fitina ya kupotea.

**Ewe Mola,** tupambe kwa mapambo ya imani, na utufanye waongofu wanaoongoza, wasiopotea wala kupoteza wengine, wenye amani kwa wapenzi wako na vita dhidi ya maadui zako. Tunapenda kwa ajili ya upendo wako na mwenye kukupenda, na tunachukia kwa ajili ya uadui wako na mwenye kukupinga.

**Ewe Mola,** nihamishe kutoka udhalili wa maasi hadi kwenye iza ya utiifu, unitosheleze kwa halali yako badala ya haramu yako, na kwa utiifu wako badala ya maasi yako, na kwa fadhila zako badala ya wengine. Ewe Uliye hai, Msimamizi wa kila jambo, Mwenye utukufu na heshima.

**Ewe Mola,** najikinga kwako na huzuni, uzito wa deni, udhalili kwa watu, uvivu, na unyonge. Na kutokana na woga na ubahili, na kutokana na madhambi na deni linalotatiza, na kutokana na kushindwa na madeni na kudhulumiwa na watu.

**Ewe Mola,** najikinga kwako na ukoma, wazimu, na maradhi mabaya.

**Ewe Mola,** Mola wa mbingu na ardhi, Mola wa Arshi tukufu, Mola wetu na Mola wa kila kitu, Muumba wa mbegu na punje, Mteremshaji wa Taurati, Injili na Qur'ani, najikinga kwako na shari ya kila mwenye shari ambaye unamshikilia kwa uwezo wako.

**Ewe Mola,** Wewe ndiye wa kwanza, hakuna kilichokutangulia; Wewe ndiye wa mwisho, hakuna kitakachokufuata; Wewe ndiye wa dhahiri, hakuna juu yako; Wewe ndiye wa siri, hakuna chini yako. Nilipe deni langu na nitajirishe kutoka kwenye umaskini.

**Ewe Mola,** Wewe ndiye Mola wangu, hakuna Mungu ila Wewe, umeniumba nami ni mja wako, niko katika ahadi yako na ahadi yako kadri ya uwezo wangu. Najikinga kwako na shari ya kile nilichokifanya, ninakiri neema zako juu yangu, na ninakiri dhambi zangu. Nisamehe, kwani hakuna anayesamehe dhambi ila Wewe.

**Ewe Mola,** naomba kwako matendo mema, kuacha maovu, na upendo wa masikini, na unisamehe na unirehemu, na ukikusudia kuleta fitina kwa waja wako, nichukue kwako bila kuathirika na fitina.

**Ewe Mola,** najikinga kwako na majaribu magumu, huzuni kubwa, hukumu mbaya, na furaha ya maadui.

**Ewe Mola,** uliyegeuza nyoyo, thibitisha moyo wangu juu ya Taa' yako.

**Ewe Mola,** usiniache na dhambi isipokuwa umenisamehe, wala dhiki isipokuwa umeiondoa, wala deni isipokuwa

umelilipa, wala haja yoyote ya dunia na Akhera ambayo inakupendeza ila umenijalia.

**Ewe Mola,** tutakabalie hakika wewe ni mwenye kusikia na mjuzi.

**Ewe Mola,** tusamehe, hakika Wewe ni Mwingi wa kusamehe, Mwingi wa rehema.

**Ee Mola wetu,** tusamehe sisi na ndugu zetu waliotutangulia kwa Imani, wala usiwe na chuki katika nyoyo zetu dhidi ya wale waliyoamini. Ee Mola wetu, hakika Wewe ni Mwenye huruma na Mwenye rehema.

**Ee Mola,** mimi ni mja Wako, mwana wa mja Wako, na mwana wa mjakazi Wako, nywele zangu ziko mikononi Mwako, hukumu Yako inatimia ndani yangu, na uamuzi Wako ni haki juu yangu. Nakusihi kwa kila jina lililo Lako, ambalo ulilijulisha kwa nafsi Yako, au ulilileta katika Kitabu Chako, au ulilificha kwa ilm ya ghaibu inayokuwepo kwako, uufanye Qur'ani Tukufu kuwa bustani ya moyo wangu, mwangaza wa kifua changu, dawa ya huzuni yangu, na kuondoa wasiwasi wangu. Ee Mola, nifundishe nisiyojua, nionyeshe nilichosahau, nipe riziki ya kukiomba usiku na mchana kwa njia inayokuridhisha, kwa rehema zako, Ee Mola wa rehema zote.



**Ee Mola,** naomba kujikinga Kwako na adhabu ya Jahannam, na adhabu ya kaburi, naomba kujikinga Kwako na fitna ya Masihi Dajjal, naomba kujikinga

Kwako na fitna ya maisha na kifo. Ee Mola, naomba kujikinga Kwako na madhambi na madeni.

**Ewe Mola,** niongoze, niruzuku, nipe afya, unirehemu. Naomba kwako kheri zote, na dua bora, na mafanikio bora, na matendo bora, na malipo bora, na maisha bora, na kifo bora. Nitie uthabiti, uzidishe uzito wa mizani yangu, thibitisha imani yangu, inua daraja yangu, kubali swala yangu, samehe makosa yangu, na nakuomba daraja za juu Peponi. Aamin.

**Ee Mola!** Nakuomba mwanzo wa kheri, mwisho wake, jumla yake, wa mwanzo na mwisho wake, wa nje na wa ndani, na daraja za juu katika Pepo, Aamin.

**Ee Mola!** Nakuomba uniinulie tajiko langu, upunguze mizigo yangu, unirekebishie mambo yangu, utakase moyo wangu, ulinde heshima yangu, uangaze moyo wangu, unisamehe madhambi yangu, na nakuomba daraja za juu za Peponi, Aamin.

**Ee Mola!** Nakuomba ubariki nafsi yangu, usikivu wangu na uoni wangu, roho yangu, umbo langu, tabia yangu, familia yangu, maisha yangu, kifo changu na kazi yangu. Kubali matendo yangu mema na nakuomba daraja za juu za Peponi, Aamin.

**Ee Mola!** Nihifadhi na Uislamu nikiwa nimesimama, nihifadhi na Uislamu nikiwa nimekaa, nihifadhi na Uislamu nikiwa nimelala. Wala usinifanye kuwa kicheko kwa adui au mwenye husuda.

**Ee Mola!** Nitenge mbali na madhambi yangu kama

ulivyotenganisha mashariki na magharibi. Ee Mola! Nitakase na madhambi yangu kama ulivyotakasa vazi jeupe linavyotakaswa na uchafu. Ee Mola! Nioshe na madhambi yangu kwa barafu, maji na theluji.

**Ee Mola!** Wewe ni Mfalme, hakuna Mola isipokuwa Wewe, Wewe ni Mola wangu nami ni mja Wako. Nimejidhulumu nafsi yangu na nimekiri dhambi zangu. Basi nisamehe madhambi yangu yote, hakuna anayesamehe madhambi isipokuwa Wewe. Niepushe na tabia mbaya, kwani hakuna anayeweza kuziepusha isipokuwa Wewe. Nipo kwa ajili Yako na nakuendea Wewe. Barikiwa na umetukuka. Ninakuomba msamaha na ninatubia Kwako.

**Ee Mola!** Najikinga Kwako nisiurudiwe umri mbaya, na najikinga Kwako na ugumu wa moyo, kughafilika, udhalili na ufukara. Najikinga Kwako na ukafiri, uovu, uasi, sifa mbaya na riya.

**Ee Mola!** Najikinga Kwako nisiurudiwe umri mbaya, na najikinga Kwako na ugumu wa moyo, kughafilika, udhalili na ufukara. Najikinga Kwako na ukafiri, uovu, uasi, sifa mbaya na unafiki.

**Ee Mola!** Najikinga Kwako na kuanguka na kuvunjika, kuzama, kuugua, na uzee wa kusumbua. Najikinga Kwako na kushambuliwa na shetani wakati wa mauti, na najikinga Kwako nisiangamie kwa kuumwa na mdudu mwenye sumu, na najikinga Kwako na tamaa inayopelekea tabia mbaya.

**Ee Mola!** Nakuomba uthibiti katika jambo hili, azma ya kufuata uongofu, kushukuru neema Yako, na ibada njema Kwako. Nakuomba moyo safi na ulimi wa ukweli. Nakuomba heri ya yale unayoyajua, najikinga Kwako na shari ya yale unayoyajua, na ninakuomba msamaha kwa yale unayoyajua, hakika Wewe ni Mjuzi wa siri zote.

**Ee Mola!** Niongoze kwenye uongofu na uniepushe na shari ya nafsi yangu, Ewe Aliye Hai, Msimamizi wa kila jambo! Ee Mola! Niongezee (neema) wala usipunguze, niheshimu wala usinidhalilishe, nipe wala usininyime, nipe nafasi ya mbele wala usinitoe, Ewe Mwenye Utukufu na Heshima!

**Ee Mola!** Nakuomba rehema kutoka Kwako ambayo itaongoza moyo wangu, itaweka mambo yangu sawa, itakusanya hali yangu, italinda aliyepo mbali nami, itainua hadhi yangu, itaangaza uso wangu, itatakasa matendo yangu, itanipa uongofu, itanilinda na fitina, na itanikinga na kila shari.

**Ee Mola!** Nakuomba afya yenye Imani, na Imani yenye tabia njema, mafanikio yanayofuatiwa na ufanisi, rehema kutoka Kwako, afueni kutoka Kwako, msamaha na ridhaa Yako.

**Ee Mola!** Wewe unasikia maneno yangu, unaona mahali nilipo, unajua siri yangu na yaliyo dhahiri kwangu, hakuna lililofichika Kwako kuhusu mimi. Mimi ni mwenye shida, masikini, mwenye kuomba msaada, mwenye kuogopa, mwenye kutetemeka,

ninayekiri dhambi zangu Kwako. Nakuomba kama anavyoomba masikini, nakusihi kama mwenye dhambi mnyonge, nakulilia kama mwenye hofu na upofu. Ombi la aliyenyenyekea Kwako shingo yake, aliyedhalilika Kwako mwili wake, aliyedhoofika pua yake. Ee Mola! Kubali toba yangu, nitakase na madhambi yangu, itikia dua yangu, nitie uthabiti katika hoja yangu, uongoze moyo wangu, unyooshe ulimi wangu, na uondoe uovu kutoka moyoni mwangu, Ewe Mwenye Rehema kuliko wote!

**Hakuna Mola isipokuwa Wewe,** Utakatifu ni Wako, hakika mimi nilikuwa miongoni mwa madhalimu.

**Ee Mola wetu!** Kwako tumekutegemea, Kwako tumerejea, na Kwako ndio marejeo yetu. Ee Mola wetu! Usitufanye fitina kwa wale waliokufuru, na utusamehe Ee Mola wetu, hakika Wewe ni Mwenye nguvu na hekima.

**Utukufu ni wa Mola wako,** Mola wa heshima, mbali na wanayomsifu kwayo. Na amani iwe juu ya Mitume wote, na sifa njema ni za Mola wa walimwengu wote.

Na sifa njema ni za Mwenyezi Mungu mwanzo na mwisho, na rehma na amani zimfikie Mtume wetu Muhammad (SAW), ahli zake, na maswahaba wake wote.

# Dibaji

Utangulizi mku ........ 4

Utangulizi ........ 6

Miakaati na Ihramu ........ 8

Tanbih (Uzinduzi) ........ 10

Nguzo, Wajibu na Sunnah za Umrah ........ 11

Nguzo za Umrah ........ 11

Wajibu wa Umrah ........ 11

Sunnah za Umrah ........ 11

Mambo Yanayoharamishwa Wakati wa Ihramu ........ 12

Sifa ya Umra ........ 15

Dua zilizochaguliwa ........ 19

Dibaji ........ 31

حرمين

رئاسة الشؤون الدينية
بالمسجد الحرام والمسجد النبوي